TUZO YA TAIFA YA MWALIMU NYERERE YA UANDISHI BUNIFU
MWAKA WA TANO - 2026/2027

VIGEZO VYA JUMLA KWA NYANJA ZOTE

- Mshiriki awe raia wa Tanzania.
- Andiko bunifu liwe katika lugha ya Kiswahili.
- Sehemu yoyote ya muswada isiwe imechapishwa na mchapishaji au kuchapishwa binafsi pamoja na kuchapishwa mtandaoni na magazetini, au kurushwa katika vyombo vya habari na burudani au kuoneshwa jukwaani.
- Mwandishi anaruhusiwa kushiriki andiko bunifu moja tu katika nyanja atakayochagua.
- Mswada utakaoshinda tuzo nyingine hautazingatiwa.
- Andiko bunifu litakalowasilishwa liwe andiko makini lililojikita katika masuala muhimu ya jamii.
- Miswada iliyoshika nafasi ya 1 - 10 katika tuzo ya miaka iliyopita haitaruhusiwa kushiriki. Hata hivyo, mwandishi anaweza kuleta muswada mwingine.

VIGEZO MAHUSUSI KWA TAMTHILIYA YA JUKWAANI

- Andiko litumie “Courier Font”, ukubwa wa herufi uwe 12
- Mswada uwasilishe wazo asili la mwandishi.
- Mswada utumie vionjo vya sanaa za maonesho za Kitanzania
- Tamthiliya iwe ya muda wa dakika 40 hadi 60.
- Tamthiliya iwe na maonyesho yasiyozidi 6.
- Wahusika katika tamthiliya wasizidi 6.

VIGEZO MAHUSUSI KWA RIWAYA

- Urefu wa riwaya uwe kati ya maneno 60,000 na 100,000.
- Andiko litumie “Times New Roman”, ukubwa wa herufi uwe 12 na “double spacing”

VIGEZO MAHUSUSI KWA HADITHI ZA WATOTO

- Hadithi ya watoto iwe kati ya maneno 250 na 1,000
- Hadithi itakayowasilishwa ilenge watoto wa miaka 5 hadi 12.
- Mwandishi aainishe hadithi yake imelenga watoto wa umri gani.
- Muswada utakaowasilishwa ujumuishe michoro.
- Kila mchoro uendane na maudhui ya hadithi.
- Mswada utumwe kama PDF.
- Hadithi itakayowasilishwa itumie lugha rahisi inayoeleweka.

VIGEZO MAHUSUSI KWA USHAIRI

- Mashairi yasipungue 50 na yasizidi 60.
- Idadi ya beti kwa kila shairi isizidi 15.

- Ikiwa mswada ni wa utenzi, uwe utenzi mmoja tu wenye beti kati ya 300-400.
- Kila shairi lipewe namba.
- Andiko litumie “Times New Roman”, ukubwa wa herufi uwe 12.

TARATIBU ZA KUWASILISHA MISWADA:

- Andiko bunifu litumwe kama kiambatisho kwa Microsoft Word kwa miswada ya ushairi na riwaya; PDF kwa hadithi za watoto; na FDX au PDF kwa tamthiliya.
- Kwa wale wenye mahitaji maalumu wanaweza kutumia Nukta Nundu.
- Kiambatisho kiwe na jina la andiko bunifu na nyanja aliyoiandikia.
- Ukurasa wa kwanza wa andiko bunifu uwe na kichwa cha andiko bunifu na jumla ya maneno au idadi ya beti kwa ushairi
- Andiko bunifu liwe na namba kwenye kila ukurasa
- Mwandishi asiandike jina lake wala taarifa binafsi kwenye andiko bunifu.
- Mwandishi aweke taarifa zifuatazo kwenye barua pepe itakayoambatana na muswada wake: Majina matatu, jina la uandishi (kama analo), jinsia, namba ya simu, anuani, wasifu usiozidi maneno 150 na umri. Usiweke taarifa hizi kama kiambatisho.
- Kila mshiriki atatakiwa kusaini tamko la kuthibitisha kuwa muswada huo ni wake na haujachapishwa mahali popote ikiwemo mtandaoni na magazetini.
    - Tamko linapataka kupitia https://bit.ly/TAMKOTUZO2026
- Andiko bunifu liwasilishwe kati ya Agosti 19 na Novemba 30, 2026
- Tafadhali tuma wasilisho lako kwa tuzonyerere@tie.go.tz

MISWADA ITAKAYOSHINDANISHWA NI ILE ILIYOZINGATIA VIGEZO. TAFADHALI HAKIKISHA UNAFUATA VIGEZO VYOTE KAMA VILIVYOAINISHWA.